JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

07 **TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO**

Muda: Saa 1: 30 **Mwaka: 2015**

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali **ishirini na tano (25)**
2. Jibu maswali **yote**

SEHEMU A: (Alama 20)

Soma swali na kisha chagua jibu lililo sahihi kati ya chaguzi nne ulizopewa na uandike herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku ulichopewa katika kila swali:

1. Simu ambazo hutumiwa na polisi ili kupeana taarifa zinaitwa

   A. simu za upepo

   B. simu za mkononi

   C. simu za mezani

   D. simu za intaneti

2. Namba ya simu ambayo hutumiwa na watu kwenye matukio ya hatari kama moto ni

   A. 113

   B. 112

   C. 110

   D. 114

3. Kifaa kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutengenezea ngoma?

   A. Plastiki
   B. Kitambaa
   C. Ngozi
   D. Mwanzi

4. Kipande cha karatasi chenye maandiko yenye ujumbe maalumu ambacho hutumika kwa matangazo ya muda mfupi kinaitwa

   A. Bango
   B. Kipeperushi
   C. Gazeti
   D. Makala

5. Kituo kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutoa ushauri nasaha hapa Tanzania?

   A. ANGAZA
   B. SHIDEPHA
   C. WAMA
   D. EMAU

6. Nyumba au chumba kinachotunza vitabu na maandiko mengine kinaitwa

   A. Maktaba
   B. nyumba ya vitabu
   C. chumba cha vitabu
   D. stoo ya vitabu

7. Kipi kati ya vifuatavyo siyo chombo cha mawasiliano?

A. Kamera

B. Radio

C. Luninga

D. Magazeti

8. Shirika la simu la Tanzania linalotoa huduma ya simu za mezani linaitwa

A. Vodacom

B. Tigo

C. TTCL

D. Nokia

9. Mwitiko maana yake ni hali ya upokeaji wa _____

A. Ujumbe

B. Maneno

C. Maelezo

D. Vitendo

10. Neno au namba za siri ambazo humwezesha mtu kufungua kompyuta huitwa

A. Kiteuzi

B. *Microsoft*

C. Faksi

D. *password*

SEHEMU B: (Alama 10)

Katika swali la 11 hadi la 15 katika sehemu hii, chagua jibu sahihi kutoka Kifungu B kama yanavyoonekana kwenye jedwali, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Na.	Kifungu A	Herufi	Kifungu B
11.	Hutumika kopokesa na kuchambua kazi zote zinazoingia kwenye kompyuta.	( )	A. Kiteuzi/mausi
12.	Hutumika kuchapa maandishi ya kompyuta kwenye karatasi	( )	B. Kibodi
13.	Hutumika kuonyesha taarifa iliyomo ndani ya kompyuta	( )	C. Spika
14.	Hutumika kuingiza maelekezo kwenye kompyuta	( )	D. Printa
15.	Hutumika kutoa sauti kwenye kompyuta	( )	E. Kichakato kikuu
			F. Skirini
			G. Ghala
			H. Diskimwako

SEHEMU C: (Alama 05)

Katika swali la 16-20 andika KWELI kama sentensi hiyo inawasilisha maudhui sahihi, na SI KWELI kama sentensi hiyo inasilisha maudhui ambayo si sahihi.

16. Mayowe hutumika katika sherehe. _____
17. Alama za barabarani huonesha namna bora ya kutumia barabara. _____
18. Maandiko yanaweza kupangwa katika maktaba kulingana na mwandishi wa andiko. _____
19. Filimbi ni njia ya kisasa ya mawasiliano _____
20. Kompyuta nyingi hutumia programu andishi ya Microsoft word _____

SEHEMU D: (Alama 15)

Katika swali la 21-25, soma swali na uadike jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi:

21. Kifaa kinachotumika kuingiza umeme kwenye betri ya simu ya mkononi kinaitwa _____

22. Barua zimegawanyika katika mafungu mawili ambayo ni barua ya kirafiki na _____

23. Hatua ya kwanza ya kutuma ujumbe kwa njia ya faksi ni _____

24. Mchoro huu ufuatao huitwa _____

